

**“WATU WOTE...”**  
**ROBERT STAPLETON**  
**Nehemia 8:1-3**

Katika fungu la maandiko litakalotumika katika makala hii (Nehemia 8:1-3), kuna kanuni ambazo zinastahili tuzizingatie.

**“NA WATU WOTE WAKAKUSANYIKA KAMA MTU MMOJA”**

Haishangazi mtume Paulo kusema alichosema katika Warumi 15:4, “Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini”. Tutajifunzaje kutokana na jambo lililoko katika Nehemia 3:1.

Imesemwa kwamba watu wote wakakusanyika kama mtu mmoja. Kwa kuwa walikusanyika Yerusalem, ni lazima tuelewe kuwa si kila Myahudi katika dini yote ya Kiyahudi alikuwepo. Walakini wale waliokusanyika Yerusalem baada ya utumwa wa Babeli walikuwepo.

Tunapata msaada wa kuelewa jambo hili kuanzia mstari wa pili. Zingatia kwamba panasema “...Wanaume na wanawake na wote walioweza kusikia na kufahamu”. Hili lingeweza kuashiria kwamba katika kundi hili Wangkuwa watoto wenye uwezo wa kusikia na kuelewa kilichokuwa kinaendelea. Mara zote Mungu ametaka watoto wafundishwe Neno lake na mapenzi yake. Huu ni mfano mojawapo ambapo walikuwa wanaletwa ili maneno ya torati kutoka kinywani mwa Ezra.

Ni balaa isiyomithili ambapo hata wale wanaodai kwamba ni waumini katika ufalme wa Mungu, wanapokataa kufanya kila wanaloeweza ili kuona watoto wao wanafundishwa neno la Bwana! Wapo watu wengi waliopotea kwa sababu wazazi wao walisababisha washindwe katika kipengele hiki. Ukweli ni ukweli! Tunaweza kujificha au tukaupokea na kuufanya kitu. Mara tuwapo katika kweli juu ya jambo hili ndivyo tutakavyokuwa na ubora kiroho sisi na watoto wetu. Kwa sisi ambao tuna watoto tunatakiwa kuona kuwa watoto wetu wanalelewa “katika adabu na maonyo ya Bwana”

**WALIKUWASANYIKA KAMA “MTU MMOJA”**

Wazo la kukusanyika kama mtu mmoja namna hii ilikuwa ni dalili ya muafaka wao. Walikuwa na muafaka katika kukunyika kwa lengo la kusikia torati ya Bwana. Kama walivyokusanyika pamoja kusikia torati ya Bwana, hakukuwa na faraka kabisa miongan mwao. Ushawishi wao uliimariswya namna hii.

Tunatakiwa kufahamu kuwa ushawishi wetu unaweza kudhoofu tunapokunyika kwa pamoja kama hatutakusanyika kama mtu mmoja (1 Wakorintho 1:10).

Ombi la Yesu katika Yohana 17 ni ombi la mshikamano kwa watu wake. Katika mst. 11, Yesu aliwaombea wanafunzi wake. Katika mst. 20-23, Aliwaombea waumini wote tangu pale na kuendelea. Kama kuna jambo linalohitajika katika ufalme wa Mungu, ni Umoja.

**WAKAMWAMBIA EZRA “AKILETE KITABU CHA TORATI YA MUSA”**

Kutokana na hili tunaona utayari wa kujifunza mapenzi ya Bwana. Bila shaka, Ezra alisoma nakala ilioandikwa kwa kiebrania na akafafanua. Katika maisha yetu tunahitaji utayari ili kuufikia uelewa wa mapenzi ya Mungu (Mathayo 5:6; 1 Petro 2:2)

**MSTARI WA TATU UNAASHIRIA JINSI WALIVYOFURAHIA KUSIKILIZA**

**NENO**– Panasema “Akasoma...tangu mapambazuko hata adhuhuri”. Hii yawezekana ilikuwa mapambazuko hadi saa sita mchana. Kama ningeingia katika “jengo lolote la kanisa” na kuhubiri kwa masaa sita unadhani ningepata muitikio gani? Unadhani ni lini ningeombwa nirudi tena?

Zingatia, watu hawa walikuwa wakisikiliza kwa makini kilichokuwa kinazungumzwa kwa masaa sita. Natambua kuwa maneno “walikuwa wasikivu” hayaonekani kwenye nakala za awali, bali yalitolewa na watafsiri. Hata hivyo, wazo la kuwapo kwa usikivu lipo katika maneno haya, “na masikio ya watu wote yakasikiliza kitabu cha torati”. Kwa hiyo, walikuwa makini na kilichokuwa kinazungumzwa.

Tunaongelea ukomo wetu wa usikivu. Hii ni sehemu ya muda ambao tunaweza kuwa wasikivu kwa jambo fulani kabla akili hajaanza kutangatanga. Kwa upande wa mafundisho au mahubiri, kwa kawaida tunasema isiwe zaidi ya nusu saa. Huoni kuwa ni jambo geni kwamba ukomo wetu wa usikivu huongezeka linapokuja suala la shughuli za kimichezo, sinema, magazeti na mengine kama hayo? Huoni kuwa ni jambo geni kwamba Wayahudi hawa wakawa na ukomo wa usikivu wa masaa sita wakati usikivu wetu ni nusu saa? Labda, nasema labda, badala ya kufikiria kuwa tuna matatizo ya ukomo wa usikivu, tuna tatizo la moyo linalotusumbua. Kwa maneno mengine, mioyo yetu iko mahali pasipo penyewe.

Sijui kuhusu wewe, lakini mimi nafedheheka ninapolifirkiria jambo hili. Pengine, badala ya kuyafanya madarasa ya Biblia na hotuba ziendane na “ukomo wa usikivu wetu,” tunatakiwa kuufanya ukomo wa usikivu wetu uendane na madarasa ya Biblia na hotuba!

Mambo mengi kama haya kutoka katika Agano la Kale yanaweza kuwa funzo kwetu. Kanuni zenye thamani kubwa zinaweza kupatikana. Tuzitafute na tuzitendee kazi maishani mwetu.